MWITO PROG 1096 KISWAHILI SCRIPT

SCRIPTURE:ROMANS 6:3

TRANSWORLD RADIO

INTRO:

Nakukaribisha tena msikilizaji wangu kwa kipindi cha MWITO nambari 1096 kutoka studio zetu za Nairobi.Sina shaka kwamba Mungu amekulinda na hata kukufikisha siku ya leo ambapo tunakutana tena.Nakukumbusha kuwa kipindi hiki kinakujia kwa hisani na udhamini mkubwa wa huduma ya kimataifa ya Macedonian Call yake Harod Williams.

Kwenye kipindi kilichopita tuliongelea akubwa kuhusu jinsi ya kuishi maisha ya ukristo.Kwa wale ambao hamukuwa nasi kweye somo lililopita tulisoma utangulizi wa sura ya 6 ya Warumi.Kumbuka mtume Paulo aliuliza swali kubwa sana ambalo tulilijadili kidogo kwenye kipindi hicho kilichopita.Naomba tusomde aya tatu za kwanza za Warumi sura ya 6 ili tuweze kuandamana vyema…. ***Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi? Hamfahmu kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake,kusudi ama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba,vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.***

Jinsi tunavyoendelea kuishi hapa duniani ,binadamu wanamwangalia Mkristo.Na ulijua kwamba hapaduniani tutakumbwa na dhiki,lakini tujitie moyo kwa kuwa Yesu aliyashina majarib na mateso.Mtumishi Petro aliyaweka vizuri sana maneno yake.Alituasa tusiwe kama watu wa ulimwengu .Kwamba tunafurahi ,mambo

yanapotuendea vizuri ,lakini wakati wa dhiki tunalamika kama walimwengu.Mtume Petro antutaka tudumishe imani na kuwa na msimamo kama mkristo halisi.Nitashangaa sana ikiwa mkristo atapima siku yake itakavyokuwa kulingana na jinsi mambo yalivyo kwenye soko la hisa.Yaani hali hiyo imwamulie ikiwa ni siku nzuri au la.Msikilizaji wangu tukiwa wakristo twapaswa kuishi maisha ya uhusiano mzuri na kristo,wala tusiyumbishwe na hali tunazopitia.

Fursa ni hii ikiwa hujamjua Kristo kuwa mwokozi wako.Ikiwa hizo hali nimetaja zinakutatiza.Kwamba huwezi kustahimili dhiki ya muda kwa ajili ya taji ya milele.Tubu dhambi zako sasa na umwendee ndugu au dada aliyeokoka na ushiriki naye kuhusu uamuzi uliofanya.Aidha mwendee mchungaji wa kanisa linalohubiri wokovu wa Yesu Kristo.Atakushauri na kukuelekeza jinsi ya kukuza imani yako. ? Utamfungulia mlango wa moyo wako ili apate kuingia?Ikiwa jibu lako ni ndio ningependa utubu dhambi zako leo na kumpokea rohoni mwako ili akue dira mpya maishani mwako.Usije ukatahayari siku ya mwisho,wakati wateule wake watakapopanga foleni kuingia Jerusalemu mpya.Mbinguni ambako tumeandaliwa makao.Chukua hatua hiyo sasa hivi.Ninasubiri uchukue hatua hiyo ,kisha uniandikie au unitumie ujumbe mfupi.Nitafurahi sana kuwasiliana nawe na ahata kukupatia vijitabu nan akala ya agano jipya la Bibilia kukusaidia kuweka msingi imara wa ukristo wako. Zaidi ya hayo.Nitafurahi sana nitakapopokea maoni yako kukihusu kipindi hiki na hasa jinsi ya kukifanya kiwe cha manufaa zaidi kwako.Hiki kimekuwa kipindi cha Mwito nambari 1096. Naomba uwasiliane nami kupitia njia ya arafa ukitumia nambari ifwatayo-: 0721 970 520. Au 020 2679842.Ikiwa unaishi Nairobi tunakukaribisha ututembelee kwenye studio zetu za TWR Kamburu Drive,off Ngong Road, baada ya jumba la TOP PLAZA.Anwani yangu ikiwa utaniandikia barua ni-:Kwa mtayarishi,Mwito,S.L.P.21514-00505 Nairobi.Waweza pia kuwasiliana nami kwa njia ya barua pepe ifwatavyo-barua@twr.co.ke.Na basi

kufikia hapo sina budi kulikunja jamvi langu kwa leo ninapokutakia baraka sufufu kutoka kwake Mungu wetu mtukuka.Ni mwaandazi wa kipindi hiki ndugu Charles Otunga ninayekuaga nikikutakia mbawazi zake Mungu wetu mtukuka.Kwaheri.

xxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxx